# USHIRIKA KATIKA UJASIRISHAJI WANACHAMA TANZANIA

**Imetolewa na**

**Suleman A. Chambo**

**Mada Iliyotolewa Kwenye Semina ya REDET kwa Viongozi wa Vyama vya Ushirika Iliyofanyika Tarehe 1 – 2 Februari 2007**

## 1. Utangulizi

Ujasirishi ni dhana ambayo imeingia katika msamiati wa ushirika hivi karibuni (Chambo 2001) hasa baada ya mjadala wa miaka thelathini ya ushirika unaosimamiwa moja kwa moja na Serikali. Mjadala huo umekuwa ukizingatia mambo mawili makubwa: Kwanza, ilijidhihirisha wazi wazi kuwa ushirika 'unaosimamiwa na serikali moja kwa moja utaendelea kuwa tegemezi na kwahiyo utashindwa kuleta maendeleo ya uchumi kwa wanachama wake. Lakini upande wa pili unaodai hoja ya ujasirishi unazungumzia hali halisi kuwa ushirika kama asasi ya wanachama, baada ya kuondoka katika uongozi wa serikali, unahitaji wanachama walioandaliwa katika uchumi wa kujitegemea. Ushirika unaojitegemea unahitaji wanachama waliojasirika.

**Ushirika una sura tatu kuu:**

Kwanza kama asasi ya wananchi wa kawaida, vyama vya ushirika vinaundwa na makundi ya watu wanaotafuta uhuru wa kiuchumi. Watafiti kama Henrics (1992) wanaafiki kuwa ujasirishi ni sehemu ya mchakato wa kutafuta uhuru wa kiuchumi kwa misingi ya haki na usawa.

Pili, ushirika ni mkakati wa mbinu za uhuru wa mamlaka na uwezo wa kuamua, ni vipi uzalishaji mali na mgawanyo wa mali zilizozalishwa ufanyike kwa kanuni za usawa, haki na demokrasia.

Tatu ushirika ni mkakati asasi wa kuwaandaa wananchi kumiliki uchumi wao kwa kutumia ushirika. Katika programu nyingi za maendeleo ya taifa, mara nyingi mkakati wa kuwandaa watu katika uchumi wa ushirika huwa haizungumzwi sana. dhana inayobebwa katika shughuli za maendeleo ni kila mwananchi na Iwake na suala la mwananchi na asasi halipo.

Katika mada hii, tutaangalia dhana ya ushirika na ujasirishaji wanachma, kwa kufanya mapitio ya mambo muhimu yafuatayo:

i) Historia fupi ya ushirika na mchango wake katika kuwajasirisha wanachama wake.
ii) Mazingira ya kisiasa na kiuchumi yaliyosaidia ushirika kuwajasirisha wanachama wake,
iii) Nguvu na udhaifu wa ushirika katika ujasirishaji wa wanachama.
iv) Tufanye nini ili kuimarisha ushirika ili utekeleze majukumu yake ya kuwajasirisha wanachama wake.

## 2. Historia Fupi ya Ushirika na Mchango wake Katika Kuwajasirisha Wanachama wake

Vyama vya ushirika nchini Tanzania, vilianza rasmi kwa kutambuliwa na sheria ya kwanza ya ushirika ya Mwaka 1932. Hata hivyo, chimbuko la msingi la ushirika, lina historia yake ambayo ilitokana na migongano ya maslahi ya kiuchumi katika uzalishaji na uuzaji wa mazao ya biashara.

Uzalishaji wa mazao ya biashara una sura tatu za kiuchumi: Kwanza ni lazima kuwe na zao linalohitajika na kundi fulani la watu. Pili zao hilo ni lazima likidhi mahitaji ya matumizi moja kwa moja ya hisia za mnunuzi. Tatu zao hilo ni lazima liuzwe kwa bei inayokubalika kwa pande zote mbili, yaani upande wa muuzaji na upande wa mnunuzi.

Hapa Tanzania, ushirika ulianzia kwenye mazao ambayo yalikuwa bidhaa moja kwa moja, yaani mazao kama kahawa, tumbaku, pamba, pareto na korosho yalizalishwa kwa ajili ya soko moja kwa moja kwa maana kuwa ni mazao ambayo yalikuwa hayahitajiki hapa Tanzania.

Lakini vile vile, ikumbukwe kuwa, Tanzania ilikuwa na mazao - bidhaa ambayo hayakuingia moja kwa moja katika mfumo wa biashara ya ushirika kama katani na chai. Mazao haya yalizalishwa na kuuzwa nje ya mfumo wa ushirika kwa kuwa mfumo wake wa uzalishaji ni wa gharama kubwa na uko nje ya uwezo wa wakulima wadogo. Mazao yaliyoingia kwenye ushirika ni yale ambayo gharama zake za uzalishji zilikuwa zinaweza kubebwa na mkulima mdogo.

## 2.1 Ushirika Katika Kupambana na Unyonyaji

Kanuni na maadili ya ushirika, vinazingatia uhuru, haki, usawa na demokrasia. . Mazao ya biashara yalipoanza kuzalishwa, wazalishaji walikuwa na matarajio ya kupata bei nzuri, hususan, ile bei inayorudisha gharama zote na kupata faida au ziada.

Kama tulivyoona, mazao yote ambako ushirika ulianzia, yalikuwa hayahitajiki hapa nchini. Kwahiyo yalitegemea wanunuzi wa nje. Kwa mantiki ya mfumo wa biashara uliotegemea şoko la nje, kulizuka kundi la wanunuzi wa kati ambao walikuwa wananunua mazao hayo kutoka kwa wakulima wadogo kwa bei ya chini na kuyauza nchi za nje kwa bei kubwa.

Kanuni moja kubwa ya mfanyabiashara wa kati ili aendelee kuishi, anahakikisha kuwa wazalishaji na wanunuzi wa mazao hawakutani na kupeana taarifa. Yeye ndiye anayehakikisha kuwa ana taarifa zote muhimu ambazo wazalishaji na wanunuzi wanahitaji.

Hata hivyo, wazalishaji waligundua kuwapo kwa unyonyaji wa bei na kwahiyo mantiki ya kusimamia uuzaji wa mazao yao kwa kutumia ushirika ulijitokeza wazi wazi. Kwahiyo ushirika wa biashara ya mazao uliundwa kutoa suluhisho la

unyonyaji ulioletwa na wanunuzi wa kati ambao wengi walikuwa wafanyabiashara wa Kihindi.

Vyama hivyo vilianzia Kilimanjaro kwenye zao la kahawa, lakini vilienea sehemu zote za Tanzania ambako kulikuwa kukizalishwa mazao ya biashara kama Mbeya, Kagera, Mtwara, Iringa, Shinyanga, Mwanza.

Mafanikio ya ushirika kabla ya uhuru yalitokana na sababu kubwa nne:

- Kwanza ushirika kuwa ni chombo pekee cha kufikia bei nzuri na kuwaepuka wafanyabiashara wa kati.
- Pili vyama vya ushirika vilikuwa vichache na vyenye wanachama na viongozi waadilifu na vilivyoendeshwa kwa misingi ya biashara
- Kulikuwa na uongozi imara uliotetea maslahi ya wanachama kwa misingi ya haki na usawa kwa ujasiri mkubwa
- Chama ambacho kilishindwa kutoa huduma za kiuchumi kwa wanachama, kilifutwa,

Matokeo yake, ushirika uliimarika sana vijijini hasa katika maeneo yaliyokuwa yanazalisha mazao ya biashara. Hata hivyo, kabla ya uhuru maeneo yaliyokuwa yanazalisha mazao ya chakula kama mahindi, mpunga na matunda au mboga hayakuwa na vyama ushirika.

## 2.2 Ushirika Baada ya Uhuru

Katika maeneo ambako ushirika ulianzia kulikuwa na uongozi wa kidemokrasia na ulioimarika. Viongozi wa ushirika walikubalika kiuchumi, kisiasa na kimaadili. Vile vile, viongozi hao, walifanya shughuli za ushirika kwa kujitolea. Wakati wa kupigania uhuru, uongozi wa ushirika ulitoa mchango mkubwa kwa uongozi wa kisiasa.

Baada ya kupata uhuru, dira na mwelekeo wa ushirika vilibadilika. Kwanza, baadhi ya viongozi wazuri wa ushirika waliingia kwenye siasa na serikalini. Pili, kwa kutambua umuhimu wa ushirika kisiasa, serikali iliamua kuwa ushirika ni

lazima uanzishwe kila mkoa, kila kijiji, hata kule ambako kulikuwa hakuna kahawa.

Mtafiti Carlsson (1992), akieleza namna ushirika wa kweli unavyoanzishwa, amehoji utaratibu wa kuanzisha ushirika kwa mbinu za ki-imla na kusisitiza kuwa ushirika wa aina hiyo hautakuwa na maisha marefu. Ameendelea kueleza kuwa ushirika wa kweli unatokana na utashi wa watu wenye dhumuni la aina moja na ya kwamba azma ya kuanzisha ushirika, inatokana na wao wenyewe na tatizo wanalotaka kulitolea ufumbuzi.Ushrika unaotokana na utashi wa watu wenyewe, huo una maisha marefu.

Utaratibu wa kuanzisha vyama vya ushirika ki-imla, ulianza baada ya uhuru na umekuwa na athari kubwa sana kwa maendeleo ya ushirika miaka iliyofuata hapo baadaye.  Lakini kwa wakati huo, mfumuko wa vyama vingi vya ushirika ulikuwa na athari za aina tatu:

Kwanza, wingi wa vyama ulileta matatizo ya usimamizi na ukaguzi wa karibu. Serikali ilijikuta ina upungufu mkubwa wa wakaguzi wa kutosha. Matokeo yake vyama vingi vilifanya kazi bila kukaguliwa. Pili, uwezo wa uongozi ulikuwa umedhoofika sana kwa sababu vyama vingi vililazimika kutafuta viongozi ambao walikuwa hawana uzoefu na elimu ya kutosha. Tatu, katika maeneo ya mazao ya chakula, watu wengi walijiunga na ushirika bila kujua wanachokitaka. Wengi walijiunga na ushirika kwa sababu Serikali iliwataka wafanye hivyo na si kwa sababu ya utashi wao wa kupambana na umaskini.

### 2.2.1 Mazingira ya Kisiasa na Kuchumi yaliyosaidia ushirika Kuwajasirisha Wanachama wake.

Ushirika tangu ulipoanza mwaka 1844, una sura ya kitabaka. Waasisi wa ushirlka wa mji wa Rochdale huko Uingereza, walikuwa ni wafanyakazi viwandani. Wafanyakazi hawa baada ya kuona unyonyaji na unyanyasaji wa wenye viwanda, walibuni utaratibu wa kiasasi, ili kutafuta mfumo mbadala wa kujipatia maslahi yao bila kupambana ana kwa ana na mabepari. Duelfer (1973) anazungumzia kuhusu madhumuni ya kuwapo kwa ushirika katika uchumi wa soko na wa kibepari. Anaeleza kuwa ushirika huwa unachukuliwa kama chombo cha kuukarabati mfumo wa kibepari. Anaeleza kuwa nia mojawapo ya ushirika

ni kufanya marekebisho na kujaza mapengo katika mfumo wa kibepari ili ubepari huo uwe na sura ya binadamu.

Kwa hiyo, ingawa waasisi wa ushirika hawakuwa na mpango wa kuubadili mfumo wa kibeparl, wallkuwa na lengo la kuziba mapengo ya mfumo huo ili watu waishi maisha bora yenye haki, uadilifu na maongozi ya kidemokrasta. Mpaka leo hii ushlrika ni sekta ya kiuchumi ambayo imeweza kuishi katika mifumo yote ya siasa uchumi kuanzia mwaka 1844.

Katika nchi kama Tanzania, ushirika haukuanzia na tabaka la wafanyakazi wanaonyonywa na mabepari viwandanl, bali ulianzia na wakulima wadogo ambao walikuwa wakinyonywa kwa kupitia bei ndogo za mazao yao waliyokuwa wanayazalisha na kuyauza kwenye soko la dunia. Ushirika wa wakati ule ulifanikwa kwa sababu kulikuwa na mazingira muafaka ya kisiasa na kiuchumi yaliyoufanya ushrika kuwa na mafanikio makubwa ndani ya wanachama wake

Ni vizuri ikabainika kuwa mafanikio ya ushirika yanapimwa kutokana na mafanikio ambayo wanachama wake wanayapata kwa sababu ya kutimizwa kwa malengo ya kiuchumi na kijamii ya ushirika huo. Wakati ushirikka ulipoanza miaka ya 1930, ulijikita zaidi kwenye mazao ya biashara ya nje, kwahiyo, mafanikio yake yalipimwa kwa wanachama kuongeza mapato yao kutokana na sera na taratlbu za blashara.

Ni kutokana na kuongezeka kwa mapato, wanachama waliimarika kiuchuml na wakapata ujasiri hata wa kuzungumza na kujenga hoja za kisiasa na za kiuchumi. Matokeo makubwa ya mapato kwa wanachama, ni pamoja na kusomesha watoto wao shule, ujenzi wa shule na ujenzi wa nyumba bora za kuishi,

Leo hii historia inaendelea kudhihirisha kuwa maeneo yatiyokuwa na vyama imara vya ushirika, wananchi wake walipata fursa ya kusoma shule hasa za sekondari kwa sababu vyama vya ushirika viliunda mifuko ya elmu ili watoto

wapate ufadhili wa kulipiwa karo ya shule. Vile vile, vyama vya ushrika villjenga shule za sekondari.

Shule ya Sekondari Lyamungo ilijengwa na vyama vya Ushirlka vya Kilimanjaro. Je, ni mazingira gani ya kisiasa na kiuchumi yaliyofanya vyama vya ushirika vikaweza kuwajasirisha wanachama wake hata wakafanya mambo makubwa ya kimaendeleo?

### 2.2.2 Mazingira ya Kisiasa

Mazingira ya kisiasa yafuatayo yalijidhihirisha katika kuimarisha nafasi ya ushinka kujasirisha wanachama wake:

**i) Sera za soko Huru na Ushirika Huru**

Ushinka ulipoanza wakati wa ukoloni, mfumo wa uchurni ulikuwa ule wa soko huru. Kanuni za uchumi wa soko huru, ni kuruhusu uundaji wa asasi za kiuchumi kama vyama vya ushinka kwa misingi ya uwezo wa kiuchumj. Vyama vilivyopata hati ya kuandlktshwa, vilikuwa vichache lakini vyenye nguvu, Hata hivyo, baada ya kuandlkishwa, ofisi ya Mrajisi wa Vyama vya Ushirika, ilivipa vyama vya ushirika uhuru mkubwa wa kutekeleza majukumu yake ya kiuchumi kwa wanachama wake.

Hata hivyo, hii haina maana kulikuwa hakuna matatizo yoyote. Matatizo yalikuwapo lakini yalipotokea, sheria ilichukua mkondo wake. Wezi wote wa mali za ushirika walipelekwa mbele ya sheria na ilipobainika ni wezi, walifungwa na kumaliza vifungo vyao walifilisiwa,

**ii) Sheria ya Ushirika inayotekelezeka Kikamilifu**

Ushinka uliweza kutoa mchango mkubwa kwa sababu uliongozwa kwa misingi ya Sheria ya Ushirika ambayo ilikuwa inafuatwa kikamilifu Hil ina maana kuwa, Ilipobainika kuwa sheria ilikuwa inavunjwa, wanaowunja walichukuliwa hatua mara moja bila kujali nafasi zao katika jarnii. Kwa misingi hiyo, utawala wa sheria katika

ushirika ulichangia sana katika kuwapa ujasiri mkubwa wanachama na kuwa na imani na ushnka

**iii) Maongozi ya Kidemokrasia na Utawala Bora**

Vyama vya ushirika ni vyombo vya kidemokrasia vinavyoongozwa na viongozi waliochaguliwa. Viongozi waliochanguliwa, wallfanya kazi zao za ushinka kwa misingi ya uadilifu mkubwa na mara nyingi kwa kujitolea.

Viongozi hawa waliongoza ushirika kwa sababu walitaka kuona mafanikio ndani ya wanachama na siyo ndani ya mifuko yao. Ni viongozi waliokuwa na uwezo wa kuwaunganisha wanachama wao kwa malengo ya muda mrefu. Ni katika kipindi hiki hiki kati ya miaka ya 1940 na 1960 ushirika uliweza kujenga mali za muda mrefu kama maghala, viwanda na hoteli. Uwezekaji uliofanyika katika kipindi hicho, haujawahi kufanyika tena katika historia ya miaka 75 ya ushinka nchini Tanzania. Miradi hii inawasaidia wanachama hadi leo ingawa mazingira yamebadilika sana ikiwa ni pamoja na kushuka kwa maadili na misingi ya utawala bora.. Mikutano mingi ya ushirika na shughuli za ushirika kwa ujurnla wake. viliongozwa kwa misingi ya uwazi, uwajibikajl na ushiriki wa wanachama katika maamuzi.

**iv) Elimu ya Ushirika na Taaluma**

Chuo cha Ushirika, chimbuko lake ni Chuo kilichoanzishwa na Chama Kikuu cha Ushirika cha KNCU kilichojulikana kama Chuo cha Biashara cha Tanganyika au "The Tanganyika College of Commerce" Chuo hiki kilichoanzia jengo Ia KNCU hadi mwaka 1968 kilipohamia eneo Ia sasa, kilitoa elimu ya ushrika kwa wanachama, waajiriwa pamoja na viongozi.

Lakini hata kabla ya kuanzishwa kwa Chuo hiki, watendaji wa vyama vya ushirika na viongozi, walipelekwa na vyama vya ushrika kupata mafunzo Chuo cha Ushirika cha Loughborough

huko Uingireza. Hli ni kwa kuzingatia kuwa elimu ni sehemu muhimu sana ya maisha ya ushirlka. Wakati huo, isingekuwa rahisi kwa mtu yeyote kupewa dhamana ya kuongoza ushirika bila kupata elimu na mafunzo ya ushirika.

Haya ni baadhi ya mazingira ya kisiasa yaliyofanya Ushlrtka ukawajasirisha wanachama wake na kupata mafanikio makubwa.

### 2.2.3 Mazingira ya Kiuchumi

Historia ya ushirika inabaini masuala muhimu ya kiuchumi yaliyofanya ushirika kuwajasirisha wanachama wake kama ifuatavyo:

**i) Nidhamu ya Kujenga Uchumi**

Ushirika ulijitokeza kama mfumo wa ki-asasi wa kupambana na mtu wa kati yaani mfanyabiashara asiyezalisha, lakini anapata mapato makubwa kuliko yule aliyezalisha. Kwahiyo ushirika ulipoanza, wanachama walikubaliana kwa kauli moja kuwa mazao yote waliyozalisha yapitie mfumo wa Ushirika. Hii ilisaidia kupunguza gharama na kuongeza mapato ya kuendesha Chama cha Ushirlka na mapato makubwa kwa wanachama

**ii) Kupunguza Gharama za Uendeshaji**

Vyama vya ushlflka vilikuwa vichache \akini vilikuwa vikubwa na vyenye uwezo wa kukusanya mazao mengi. Vile Vile, Viliajiri watendaji wachache wenye uwezo na waaminifu. Ununuzi uliweza kufanyika kwa kukusanya mazao bila malipo ya fedha taslimu kwa sababu mantiki yake ilikuwa wanachama wakusanye mazao yao chama chao cha ushirlka kitafute mnunuzi mwenye bei nzuri kupitia wanunuzi wengine. Kwa njia hii, vyama vya ushrika viliweza kuuza mazao yao kwa bei nzuri na kuwapatia wanachama wao mafao ya kutosha.

**iii) Usindikaji wa Mazao ya Kilimo**

Uchumi wa vyama vya ushirika vya mazao uliendana na usindlkaji wa mazao ili kwanza kupunguza uzito wakati mazao hayo yakisafirishwa kwenda nchi za nje. Lakini vile vile, usindikaji wa mazao uliongeza

thamani ya mazao hayo kwa kiwango kikubwa. Mazao kama pamba, kahawa na tumbaku yalifanyiwa usindikaji wa mwanzo na kuongeza thamani ambayo kutokana na uaminifu uliokuwapo ongezeko Iolole Ia mapato iliwafikia wanachama.

**iv) Huduma za Kiuchumi**

Ushirika ulianza na mazao ya kilimo, kuongeza uzalishaji na ubora wa mazao, vyama vya ushirika vilikuwa na jukumu Ia kutoa huduma za kiuchumi kwa wanachama wake. Pembejeo, zana za kilimo na huduma za ugani vilipatikana katika muda muafaka na uzalisjhaji uliongezeka na wanachama kuongeza mapato. Hata hivyo, ieleweke kuwa huduma hizi hazikuwa za bure.

v) **Huduma za Fedha**

Vyama vya ushirika vilikuwa na utaratibu rasmi wa kutoa huduma za fedha kwa wanachama wake. Wanachama waliohaitaji mlkopo ya uzahshaji wa mazao ya kilimo walipata mikopo hiyo kwa urahisi. Vile vile, fedha za kununulia maza ziliweza kufika vijijini bila matatizoo yo yote. Ushirika ndiyo taasisi peke yake iliyoanza kupeleka fedha nyingi vijijini, hivyo, kusaidia ujenzi wa Uchumi wa fedha. Pamoja na hayo, vyama vya Ushirika vilunda benki yao iliyojulikana kama ‘The Co-operative Bank of Tanzania’. Benki hii ilifanya kazi nzuri sana ya kutoa huduma za fedha kwa wanachama hadi ilipovunjwa mwaka 1968.

## 3 Nguvu na Udhaifu wa Ushirika katika Ujasirishaji wa Wanachama

Katika historia ya Ushirika hapa Tanzania, ujasirishi wa wanachama ulikuwa mkubwa sana kabla ya uhuru na kipindi kifupi baada ya uhuru hadi 1966. Baada ya hapo, Ushirika uekuwa ukikumbwa na matatizo ya nje na ndani yake ambayo yamefanya ushirika upoteze nguvu ngingi za kuhimili ushindani katika soko. Haya yote, ni muhimu sana tukatambua nguvu na udhaifu wa Ushirika ili kubaini mkakati gani ufanyike kuunusuru Ushirika nchini Tanzania.

## 3.2 Nguvu ya Ndani ya Ushirika

Ushirika unazo nguvu za msingi ambazo kama zitaibuliwa vizuri, Ushirika unaweza kuanza kupiga hatua za kimaendeleo. Nguvu hizo ni kama ifuatavyo:

**i) Wanachama**

Nguvu ya Ushirika wowote ule ni wanachama wake wanaume na Wanawake. Lakini wanachama wanahitaji mambo matatu makubwa kama tunataka ushirika ulio na nguvu zaidi. Kwanza, wanahitaji elimu, wanachama wanahitaji elimu ya ufahamu wa ushirka, nafasi yao katika Ushirika na elimu ya biashara ili wawe wajasiriamali pale walipo katika mazingira yao ya uzalishaji.

Pia, wanataka ushiriki wa majukumu na shughuli zote za maamuzi ya biashara yao. Suala la ushirikishwaji wanachama linahitaji viongozi ambao wana upeo mkubwa na wanakubali kuwashirikisha wanachama wao moja kwa moja.

Tatu, nguvu za wanachama zınatokana na wıngı wao. Ushınka utakuwa na nguvu kama idadi ya wanachama itakuwa kubwa, sautı ya walio wengi ınasıkıka zaıdı kulıko ya wachache.

**ii) Uchumi**

Nguvu ya ushrıka inatokana na watu kuıngia katika uchumı vikundi. Faida moja kubwa ya uchumi vıkundı ni uzalishaji unaofanyıka kwa gharama nafuu na kwa hivyo kupata mapato makubwa kutoka kwenye şoko. Mzalishaji mmoja mmoja hataweza kuingia katika ushindani wa şoko kwa gharama nafuu. Kwa mantiki hii ya uchumi vikundi, wanaushırıka wanapata kinga ya gharama na kinga ya bei katika mfumo wa seko la ushindani.

**iii)Kanuni na Maadili ya Ushirika**

Ushirika ni mfumo wa biashara unaoendeshwa kwa misıngı ya kidemokrasia. Kanuni hizo zinazungumzia haki na wajibu wa kıla mwanachama katika shughuli za ushirika. Wanachama wana hakı zao za msingi na wana wajibu kwa chama Chao cha ushirıka. Kwa mantikı

ya miongozo ya kidemokrasia, kila mwanachama anashirikishwa katika maamuzi mbalimbali ili ahusike moja kwa moja na maendeleo ya ushırıka wake.

Kutokana na kanuni zake za biashara inayoendeshwa kidemokraisa, ushirika ni asasi ambayo ikifahamika vizuri, inakubalika kwa haraka ndanj ya jamii.

## 4.2 Udhaifu wa Ushirika

Ushirika umeshindwa kuwajasirisha wanachama wake kutokana na mazingira ya kisiasa, kiuchumi na kijamii ambayo umekutana nayo hasa baada ya uhuru. Maeneo ya udhaifu wa ushirika ni kama ifuatavyo:

### i) Uongozi Hafifu

Sera ya ushirika ya mwaka 2002 inatambua kuwa, viongozi wa zama za sasa wameshindwa kuongoza mabadiliko makubwa yanayotokea katika uchumi şaşa hivi. Hii ni kwa sababu, tangu sera za uchumi wa soko zilipoanza, viongozi hao hawakuyaona mabadiliko ya soko yalivyokuwa na maana mpya katika mfumo wa soko huru. Kwa mfano, kwenye ushirika wa kuuza mazao ya kilimo, vyama vikuu vingi vilifikiri, vyama vya msingi vingeendelea na kukusanya mazao na kuyakabidhi kwenye vyama vikuu kama zamani. Hili halikuwa sahihi. Baada ya kushindwa kulichambua soko kikamilifu baadhi ya vyama vikuu vilianza kuzorota na kushindwa kuwajasirisha wanachama.

### ii) Mfumo wa Ushindani katika Soko

Mameneja na watendaji wengine nao walifikiri mfumo wa soko ungeendelea kama zamani wakati wa soko la ukiritimba. Waltpoona mazao hayaji kwa wingi kutoka vyama vya msingi waliamua kufungua vituo vya kununua mazao karibu na vyama vya msingi, hivyo kuashirla ushindani wa kibiashara ndani ya ushirika. Hii imeleta uzorotaji mkubwa wa kutoa huduma kwa wanachama.

### iii) Usimamizi wa Serikali

Sheria ya ushirika ya mwaka 2003 imeendelea kuhodhi madaraka ya vyama vya ushirika. Ingawa kuna maeneo yanayoonyesha nia ya kuviachia vyama vya ushirika uhuru wa biashara, Yado kuna sehemu

zinaonyesha serkali kuendelea kuhodhi madaraka ya vyama vya ushirika.

Sheria ya ushirika ina sehemu kuu tatu:

Kwanza ni sehemu ambazo ni za taratibu za kisheria za kuandikisha vyama vya ushirika. Sehemu ya pili inahusu utawala ndani ya vyama vya ushirika. Sehemu ya tatu ni kuhusu biashara na usimamizi wa ushtrika ambayo vyama vya ushirika bado vinabanwa na serikali. Mazingira haya ya kisheira, yanaashiria vyama vya ushirika kushlndwa kuwajasirisha wanachama wake.

iv) **Ushirika Tegemezi**

Kiptndl cha biashara huru, ni kipindi cha taasisi kujtendesha zenyewe. Pamoja na kuwa mazinyra ya biashara yamebadlllka, klutendajl, vyama vya ushrika bado vinaltegemea serikali.

Kwa Vile baadhi ya wanasiasa wamekuwa wakltumta nafasl zao katlka ushirika kujipatia nafasi za kisiasa, rasimu ya sheria ilipojadlliwa Bungenl, kifungu kilichokuwa kinazungumzia kuwanyima wanasiasa kut011hussha na uongozi wa ushirika kilipofika Bungeni, kiliondolewa. Laklnl kwenye sera ya ushirika kinaendelea kubaki.

Hiki ni kiashiria kimojawapo kinachoonyesha kuwa, ushirika bado unahitajika kwa malengo zaidi ya yale ya kiuchumi.

Kuvilazimisha vyama vya ushirika vya akiba na mlkopo kutekeleza majukumu ambayo si ya vyama hivyo kwa mfano kuvitunma vyama htvyo kugawa pembejeo za kilimo, ni kuvidhoofisha. Vyama hlvyo viliundwa kufanya kazi za kuunda mtaji fedha na kukopesha wanachama. Hiyo ndiyo kazi yake. Vyama vya ushrika vya kuuza mazao kazi yake majawapo ni kugawa mbolea kwa mkopo na baadaye kurudisha mkopo huo wakatl wa kuuza mazao kwa utaratibu unaoeleweka.

**v) Wadandiaji wa Ushirika**

Kipindi cha uchumi wa soko huru, vyama vya kuuza mazao ya killtno kumetokea kundi Ia watu ambao si wanachama wa hisa, lakini wanapata

huduma zote za chama cha ushrika bila gharama yeyote. Watu hawa m wadandiaji wa vyama vya ushirika. Matokeo yake, wako watu wengi ambayo wamekuwa wakitumia huduma za ushirika na wameachwa kuviletea vyama vya ushirika gharama kubwa. Kuna sababu nyingt ambazo zinaweza kutolewa kuhusu hali hii lakini tatu ni za msingi, Kwanza inaonyesha jinsi ambavyo sheria na kanuni za vyama vya ushirika zinavyoweza kuvunjwa kwa urahisi na hakuna linalotokea. Pili, inaonyesha jinsi ambavyo sura ya namna ambavyo ushirika hauna mwenyewe. Tungekuwa na wanachama waliojasirlka, Ingekuwa rahisi kuwazula wadandiaji na kuwaelemtsha wawe wanachama, ill wapate huduma ambazo wanalipia gharama. Tatu Inadhlhirisha udhatfu wa viongozi wa ushirika wanaoruhusu wadandjaji ill kuongeza makato ambayo yanabaki kwenye chama kwa sababu wadandiaji huwa hawapati malipo ya mwisho. Hata hivyo, hakuna anayefanya ullngantsho wa mapato yanayotokana na wadandtaji na gharama zinazotokana na kuwapa huduma. Carlsson: 1992 anaeleza kuwa katika mojawapo za sababu zinazodhoofisha ushirika katika Bara la Afrika, ni mitaji midogo ya vyama vya ushirika kuhudumia wadandiaji ambao hawako tayari kulipia gharama yeyote, ili mradi wapate huduma za bure.

5. **Mstakabali wa Kuimarisha Ushirika ili Utekeleze Majukumu yake ya Kujasirisha Wanachama**

Chama cha Ushirika ni muungano wa kikundi cha watu walioungana na kuunda asasi ya kiuchumi ambayo wanashirikiana kuigharamia, kuisimamia na kugawana wajibu na mafao kwa misingi ya usawa, demokrasia na kujitegemea vyama vya ushirika ni asasi, mchakato na mkaakati wa kujenga uchum wa kitaifa kwa kutumia nguvu za wananchi wenyewe kwa misingi ya kujitegemea Ujenzi wa ushirika imara ni mkakati huru unaoashiria, kusaidia na kuunga mkono mkakati wa kitaifa wa kukuza Uchumi na kupunguza Umaskini.

Hata hivyo ujenzi na usimanmzi wa ushirika ili uweze kuwajasirisha wanachame Wake, ni lazma utizamwe upya ki-asasi, ki-sera, ki-demokrasia na kl-muundc Mikakatl Ifuatayo ni vizuri ikapewa nafasi ya utekelezaji ili kupata sura mpya ya ushlrlka mpya unaojasirisha wanachama wake.

## 5.1 Ukarabati na Uboreshaji wa Mifumo ya Ushirika uliopo

Ushl(lka ultopo sasa hivi ni ushirika mchanganyiko dunl na ushirika ugavt. IJshlrlka mchanganyiko duni ni ushirika ambao haukujipanga kuleta maendeleo kamillfu kwa wanachama wake. NI ushirlka mchanganyiko kwa sababu vcpo vyama Imara, vyama haflfu, vyama sinzia, vilivyokufa na vinavyoanza. Wakati tuna ushirika mchanganyiko wa namna hii na pamoja na kuwa kuna Mpango kabambe wa Maboresho na Modanaizesheni ya ushinka. Mpango kabambe huo na aina yake katika Bara la Afrika, utekelezaji wake tangu 2005 unaonyesha bado unasua sua pamoja na nia nzuri ya serikali mpaka hakuna vitendo vya wazi wazi vinayoonyesha azima ya kufufua upya vyama vya ushirika na miundo yake,

Carlsson 1992, ametoa maainisho mawili ya aina ya miungano ya kitaifa ya ushirika na akaonyesha kuwa kuna ushirika ugavi na ushirika unganishi. Ushirika ugavi ni ule ambao upo kwa sababu ya malengo ya kurahisisha huduma au bidhaa kugawanywa kwa urahisi. Ushirika wa aina hiii haukui na vyarna vyake vya msingi havina uhusiano lala bali vina uhusiano wima tu kwa vile mamlaka au asasi fulani za kitaifa zipo kutoa huduma.

Ushirika unganishi ni ushirika ambao vyama vya msingi vina uhustano lala na wima kwa pamoja na una malengo ya kuleta mabadlliko katlka Jamil kwa kuchangia kwa nguvu mabadlliko na maboresho ya sera.

Ushirika wetu Tanzania una sura ya ushirika ugavi. Tunahitaji mikakati ya ujenzj wa ushirika unganishi kwa kujenga mitandao ya vyama vya vingi kuanzia chini hadi ngazi ya taifa. Kazi hii ni kubwa na inahitaji muda lakini ni ya msingj kama tunataka kuona ujasirishi wa wanachama wa ushirika.

**Kielelezo Na 1** hapa chini, kinafanunua ana za ushlrika ugavi na ushl(ika mtandao au ushirika unganishi.

| Ushirika ugavi | Ushirika Mtandao (Uhanishi) |
| --- | --- |
| **Vyama vya Msngi Kitaifa** | **Vyama vya Msingi vinajenga mtandao Vijini na** |

Tunahitaji mkakati wa ukarabati na maboresho kuuondoa ushirika kutoka mfumo wa ugavi na kwenda mfumo unganjshi au mfumo mtandao.

## 5.2 Ukarabati wa Kiasasi wa Vyama vya Ushirika

Mazingira ya kiuchuml nje ya vyama vya ushlnka yanabadilika kwa kasi kubwa sana kuliko mabadiliko yanayotokea ndani ya Ushirika. Kwa mantiki hiyo, kila chama cha Ushirika kinahitaji kurejea mfumo wake wa sasa na kuandaa mfumo mpaya ambao unaenda na mahitaji mapya ya wanachama wa zamani na yale ya wanachama wapya (Organizational Transformation baada ya mipango ya kupunguza gharama tu).

## 5.3 Ukarabati wa Taasisi zinazotoa Huduma kwa Vyama vya Ushirika

Katika ujenzi wa Ushirika na Ushirika jasirishi, ni lazima kuwe na mabadiliko makubwa (Organizational Transformation) katika taasisi zinazotoa huduma za ugani, elimu, mafunzo na ukaguzi. Taasisi hizo ni Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika hususan idara ya Ushirika, Chuo Kikuu Kishiriki cha Ushirikana Biashara hususan Taasisi ya Elimu ya Endelevu na Maendeleo ya Ushirika. Taasisi hizi zina mifumo ya zamani ya ki-taasisi na taratibu za zamani ambazo zinatakiwa zibadilishwe ziende na mahitaji ya kusaidia ujenzi wa Ushirika shirikishi na jasirishi. Bila mabadiliko hayo, miundo ya zamani ya taasisi hizo itaanza kuwa kikwazo cha maendeleo ya ushirika mpya.

## 5.4 Kuongeza Idadi ya Vyama vya Ushirika na Wanachama

Ili ushirika uweze kuchukua nafasi yake katika ujnezi wa Uchumi wa Taifa na ksuhiriki katika kuchangia mkakati wa kukuza uchumi na kupunguza umaskini wingi wa vyama vya ushirika na wanachama waliojasirika ni hoja za msingi.

Hata hivyo, katika mkakati wa kuongeza wanachama na vyama vipya,hatua zifuatazo katika kuandkisha na kufuta vyama vya ushirika na uhamasishaji wa uanzishwaji wa vyama vipya vya ushirika zinapendekezwa.

Sera ya ushirika inazungumzia kupanua wigo wa kuanda vyama vya ushirika kwenye sekta mbalimbali za Idara na Wizara za serikali. Lakini hii hawezi kutokea kama uhamasishaji na uanzishwaji wa vyama vya vipya vya Ushirika utaendelea kufanywa na serikali. Vile vile, kupanua wigo hakuwezi kuharakishwa kama uandikishaji na ufutaji wa vyama vya Ushirika utaendela kufanywa na ofisi ya Mrajis mmoja nchi nzime na wasaidizi wake mikoani.

Inapendekezwa ifuatavyo:

a) **Kuhamasisha Uundwaji wa Vyama Vipya vya Ushirika**

Kazi hii ifanywe na shirikisho la vyama vya ushirika au vyama vya kitaifa vya Akiba na Mikopo. Viwanda na Mitambo mengine ya ushirika Senkali inaweza kusaidia kutoa fedha za uhamisishwaji wa ujenzi wa vyama vipya vya ushirika. Serikali ikiendelea kuanzisha vyama vya ushirika itarudisha hisia za ujenzi wa vyama vya ushirika vya serikali. Matokeo yake ni kuwa na ushirka tegemezi na Ushirika ugavi, has katika mazingira ya jamii inayongojea kufanyiwa kila kitu cha maendeleao na serikali.

b) **Mamlaka Ya Kuandlkisha na Kufuta vyama vya ushinka**

Ili kupunguza msongamano na ukiritimba, ofisi ya kuandikisha vyama vipya na kuvifuta, isambazwe ofisi za wizara zote na ngazi ya Kata. Zoezi la kuandikisha au kufuta linatakiwa lisiwe gumu sana mbele ya wananchi

wenye nia ya ujenzi wa ushirika shirikishi na jasirishi. Hii haina maana tunapendekeza uundwaji wa ushirika utitiri usifuata misingi ya shena na kanuni za ushirika. La hasha, tunachopendekeza ni kuwa wataatam wa kuandikisha vyama vya ushirika watasimamiwa ra Mrajis wa vyama vya Ushirika ambaye pa kazi zake nyingine kubwa ni kutengeneza taratibu muafaka na shirikishi za kusimamia ubora wa vyama vya Ushirika. Vile vile, hii itasaidia azma ya serikali ya kuanzisha na kuongeza idadl ya vyama vya ushirika kwenye sekta nyingine ambako ushirika haujulikani sana kama kwenye madini, ufugaji, ujenzi wa nyumta bora na uvuvi,

### 5.5 Elimu ya Ushirika Jasirishi

Mapokeo ya elimu ya ushirika na mafunzo yamejenga hisia kuwa ushirika ni taratlbu za kufanya biashara na shughuli za kiuchumi kwa misingj ya haki, sheria na demokrasia.

Lakini watafiti wengi hasa Ira Shor na wenzake; 1994, wamehoji aina ya elimu ya ushirika inayotolewa kwa viongozi na wanachama kuwa haiwaandai wanachama na viongozi kubadilisha mifumo iliyopo na inayowapunguzia nguvu za ujasiri. Mifumo ya elimu ya ushirika haiwaandai wanachama kujikomboa, bali inawapa taarifa za kawaida za uzuri wa ushirika, utunzajl wa vitabu, uchumi, n k. na kuwaambia wawe wapole, wasijenge hoja, wasipige kelele na wawe watulivu na wakimya.Ukimya umekuwa adui mkubwa sana wa ushirika Mkutano wa viongozi wa ushirika wa Afrika uliofanyika Arusha Tanzania mwezi Oktoba 2006, ulizungumzia kwa kirefu kuhusu vyama vya ushirika kushindwa kueleza na hata kuandika mafanikio yao. Ilionekana wazi wazi kuwa vyama vya ushirika vinaona aibu kuzungumza hata pale ambapo vina hoja nzito ndani ya jamii.

Lakini mwandishi Henricks; 1995 akiandika kuhusu dhana ya ujasirishi anakubaliana na Levin: 1995 kuwa ujasirishi ni mchakato ambao madaraka ya kuamua yanawashirikisha watawaliwa au wanachama. Ujasirishi uko katika awamu ya mbili:

Kuna ujasirishi binafsi ambao ni uwezo wa mtu binafsi kuhojia na kujipatia madaraka binafsi katika jamii. Ujasirishi binafsi hauna maana kubwa ndani ya vyama vya ushirika kwa sababu umetumika kuwakweza baadhi ya viongozi wakapata madaraka na kuyatatumia vibaya.

Awamu muhimu ya ujasirishi ni ile ambayo Henrick:1995, anaiita ujasirishi halisi (objective empowerment). Huu ni ujasirishi unaolenga kuleta mabadiliko makubwa katika jamii kwa sababu unawahusu watu wengi na makundi makubwa ya wananchi.

Ujasirishi huu ndio unaotakiwa kwenye ushirika kwa sababu unalenga kat:ka hatua muhimu tatu (Henrick; 1995): Kwanza ni ufahamu wa ujumla kuhusu haki, wajibu na mafao. Pili, ni haki ya ushiriki wa wanachama katika kuzalisha mali na tatu ni ushiriki wa wanachama katika kuondoa vikwazo vya mifumo ya utawala na vya utendaji, ili kuongeza tija na mafao yao, Kwahiyo kwa mantiki ya yapo juu, ujasirishi siyo hisia peke yake au mabadiliko kifikira tu, bali ni pamoja na kuleta mabadiliko yanayoonekana katika mifumo ya ugawaji wa madaraka na mafao.

Kwahiyo mkakati wa kutoa elimu ya ushirika na mafunzo, ni lazlma ufungamanishwe na dhana ya ujasirishi. Bila kufanya hivyo tutatoa wahltjmu ambao wataendeleza mifumo iliyopitwa na wakati. Hii ndiyo sababu moja kuu ya kupandishwa hadhi Chuo cha zamani cha Ushirika na kuwa Chuo Kikuu Kishirika cha Ushirika na Biashara ili tuanza kuzalisha wahitimu ambao ni wabunifu na watakaosimamia mabadiliko makubwa katika ushirika na ujasirishi kama nafasi yao halisi katika historia ya ushirika nchini mwetu.

## 6. Hitimisho

Wanachama waliojasirika. ni chimbuko muhtrnu sana la ushjrtka endeievu kuwa na ushirika jastnshl, mikakatl kadhaa tnahltajlka ambayo nt pamo;a na ukarabati wa mifumo ya shirlka. ukarabati wa taasjsi za senkatl na kuungantsha na kufungamamsha elmu ya ushlrlka. mafunzo na ujastnshl,

## REJEA

Carlsson, A Co-operatives and the State: Partners in Development? Institute of International Education, Stockholm University, Stockholm, 1992

Chambo, S.A " Experience of the MEMCOOP Project in Tanzania- Paper presented at a conference on Co-operative Development and Change in Africa Norwegian Society for Development, Oslo, Norway, November, 2003

Duelfer, E, Operational Efficiency of Agricultural Co-operatives in Developing Countries" In Carlsson, A ibid

Henricks, J " Empowerment Practice and Social Change: The Place for New Social Welfare Movement and Community Organizing Conference, University of Washington, Seattle, Washington, November, 1-3 1995

Kevin, D Empowerment: Theoretical Background and Application, CSWT Papers, Washington, 1995

Shor, I. Empowering Education Critical Teaching for Social Change University of Chicago, Chicago,2003.